SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.24 NO. 1 2025
DOI: 10.51984/JOHS.V24I1.3710

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs

# KISIWA CHA PEMBA ZANZIBAR

Ali Idris Ali Aburima

Department of Languages and African Studies, Faculty of Languages, Sebha University, Libya

**Keywords:**
Kisiwa
Pemba
Afrika mashariki
Utamaduni
Jamii

**A B S T R A C T**

This Makala hii inahusu Kisiwa cha Pemba kilichopo katikati ya Bahari ya Hindi, ni sehemu ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar katika Tanzania. Umbali na Tanganyika au Tanzania bara ni 50 km. Kimejulikana kwa muda mrefu kuwa ni kati ya miji ya kale ya kibiashara katika pwani ya Afrika ya Mashariki. Katika makala hii inabainisha umuhimu wa kisiwa cha Pemba katika Afrika mashariki na mambo mbalimbali kama: Hali ya hewa, mimea ya asili, kilimo, kazi, huduma za jamii na mwasiliano.

# جزيرة بيمبا الزنجبارية

علي إدريس علي أبوريمة

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية اللغات، جامعة سبها، البلد ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
جزيرة
بيمبا
شرق إفريقيا
الثقافة
المجتمع

**الملخص**

هذه المقالة تسلط الضوء علي جزيرة بيمبا التابعة لجمهورية تنزانيا الإتحادية، وتبعد عن ساحل تنزانيا بحوالي 50 كيلومتر، وتعتبر هذه الجزيرة ذات أهمية كبيرة نظرا لموقعها المهم، الذي مكنها أن تكون حلقة وصل بين دول شرق أسيا وافريقيا، من خلال مرور السفن التجارية عليها.
وقد تناولت المقالة أمور مختلفة تتميز بها هذه الجزيرة وهي : الحالة الجوية، أهم المحاصيل، سوق العمل، الخدمات، وسائل المواصلات.

## UTANGULIZI

Kisiwa cha Pemba kiko umbali wa maili arobaini (40) kutoka Bara.Pia kutoka Zanzibar hadi Pemba ni maili 29. kwa urefu kisiwa hiki kina maili 40 na upana ni maili 14.
Kisiwa hiki kimezungukwa na visiwa vingi vidogo vidogo. Katika visiwa hivyo vyengine ni makazi ya watu na vyengine havikaliwa. Mfano wa visiwa hivyo ni Fundo, Makoongwe, Njao,Uvinje, Kojani na kadhalika. Kwa mujibu wa ramani ya kisiwa cha Pemba visiwa vingi vidogo vinaonekana kaskazini ya Pemba.

## HISTORIA FUPI YA KISIWA CHA PEMBA

Kisiwa cha Pemba kama ilivyo sehemu nyengine za dunia, ilikuwa na tawala zake za jadi. Mtawala mkuu alijulikana kama mkamandume. Kuwepo kwa tawala hizi kunadhihirisha wazi kuwa jamii za watu wa Pemba hazikuwa tulivu lakini ziliendelea hadi kufikia hatua ya umwinyi.
Kulingana na nadharia ya Marx umwinyi ni mfumo wa tatu wa maendeleo ya mwanaadamu ukitanguliwa na ujamaa wa kale. Utumwa na baadae umwinyi.
Wakazi wa kisiwa hiki wanakadiriwa kufikia laki nne Asilimia tisini na tisa (99.9) ya wakazi wake ni Waislamu wenye madhehebu ya Sunni na lbaadhi. Inakadiriwa kuwa uislamu katika kisiwa hiki uliingizwa na wageni wa mwanzo waliofika Pemba kwa lengo la kufanya biashara.
Pemba ilivamiwa na wageni wengine katika nyakati tofauti. Mfano wa wageni waliovamia Pemba kwa lengo na kutawala ni wareno kame ya kumi na saba (17). Kama historia inavyoeleza Wareno walitimuliwa na waarabu ambao baadae waliweka maskani ya kudumu.
Asili ya watu wa Pemba inasadikiwa kuwani kutoka bara. Hata hivyo inakadiriwa kuwa watu hawa walifika kisiwani Pemba miaka mingi iliyopita. Watu hawa walitokea Kenya (wagunya) ambao walifika Pemba kwa shuguli za kiuvuvi, washihiri ambao walitoka Bara Ajemi inasadikiwa kufika Pemba kwa shuguli za kibiashara iliyoshamiri zaidi katika kame ya saba. Wengine ni watu wa asili ya mrima (Tanzania Bara) hawa walifika Pemba kwa kupitia biashara ya utumwa iliyonawiri wakati wa utawala wa waarabu kutoka Oman katika karne ya kumi na tisa. Wakati huu watumwa ndio iliyokuwa nguvu kazi kubwa katika mashamba ya karafuu na minazi .
Kutokana na muingiliano huo hivi sasa watu wa Pemba ni machotara yaani ni mchanganyiko wa makabila mbali mbali. Hata hivyo wenyeji wa Pemba hivi sasa ni watu wenye makabila kama al-maul, al-bajun, masharifu, wagunya na kadhalika. Licha yakuwa watu wa Pemba ni wenye makabila mbali mbali watu hawa wanaustaarabu wa pekee. Mfano kupenda wageni, kusaidiana wakati wanapokabiliwa na matatizo mbali mbali kama misiba na kadhiya nyengine za kijamii**.** Kutokana sifa hii ya watu wa
Pemba kisiwa hiki kimejizolea ajfa nyingi na kupata umaarufu mkubwa kwa wageni.
Waarabu waliendelea kuishi kisiwani Pemba na kumiliki njia kuu zote za uchumi hadi 1964 kiutawala, baada ya Mapenduzi ya 1964 Januari, Pemba imegawanywa katika mikoa miwili. Mkoa wa

*Corresponding author:
E-mail addresses: Ali.aburima@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 13 December 2024 - Received in revised form 30 January 2025 - Accepted 13 February 2025*

kaskazini na Mkoa wa kusini.

Mkoa wa kaskazini una wilaya tatu nazo ni wilaya wa Wete, Micheweni na wilaya ndogo ya Kojani.

Mkoa wa kusini una wilaya ya mkoani na wilaya ya Chake Chake. Mkoa wa kaskazini unaongozwa na mkuu wa mkoa ampaye ni Mheshimiwa Faki Dadi Faki. Mkoa wa kusini uko chini ya Mkuu wa mkoa Mheshimiwa Juma Kassim Tindwa.

**UTAMADUNI NA MICHEZO**

Utamaduni ni kielezo chajamii. Kwa kutumia utamaduni mtu anaweza kuitafautisha jamii Fulani.

Utamaduni unajumulisha mambo mengi. Mifano wa mambo hayo ni :-

1. Lugha
2. Ngorna
3. Michezo na kadhalika

Katika k.isiwa cha Pernba suala la utamaduni ni jarnbo ambalo linawavutia wageni wengi. Kwa upande wa lugha watu wa Pemba huzungumza lahaja ya Kiswahili ambao hujulikana kama lahaja ya kipemba.

Kwa upande wa ngorna ni ngoma ya Msewe ambayo huvuta haiba ya watu wengi wanaiangalia. Msewe asili yake ni mchanga mdogo ambayo iko mkoa wa kusini, wilaya ya Wete. Ngoma hii hupambwa kwa mdundo wa ngoma na nyimbo za kifasihi, rnfano wa nyimbo moja ya Msewe :-

"Ukinipenda usinipende nina m.ume wangu jembe"

Hii ni nyimbo inayosisitiza utendaji wa kazi. Kwa ufupi ngoma ya Msewe huchezwa wakati wa sherehe za kitaifa, harusi na kadhalika.

Kwa upande wa michezo, mchezo wa ng'ombe ni maarufu sana kisiwani Pemba. Mchezo unasadikiwa uliletwa wakati wa utawala wa kireno katika karne ya kumi na saba. Kama michezo mingine, mchezo huu huchezwa wakati wa sherehe muhimu za kitaifa.

**RAMANI YA PEMBA**

Ni kisiwa kilichojulikana ulimwenguni tangu karne nyingi zilizopita, kisiwa hicho kilikuwa chini ya mamlaka ya sultani wa Oman tangu karne ya 17. kisiwa hiki kilijitarnbulisha haraka duniani kutokana na utajiri wake wa viungo. Asilimia 90 ya karafu zote duniani zilitoka Pemba.

**UMBILE**

Kutokana na ushahidi wa ramani. Kisiwa cha Pemba kina mwambao wa pwani ulio songombingo. Ardhi yake mwanda ulio tambarare. Hii ni sehemu ndogo tu kisiwa cha Pemba. Eneo miinuko na yenye kufikia hadi mita 104 au futi 311 mfano kisongom- Mkoani. Katika upande wa mashariki na kusini kisiwa hiki ni uwanda wajiwe.

Pemba ina mito mingi na mingi ya mito hiyo ni yenye kukauka wakati wa kiangazi na michache ni mito ya kudumu. Mfano wa mito a kudumu ni mto weni (Wete), Chamanangwe (Mchanga mdogo) na kwapeza (Chake Chake Dutani). Pia yapo maziwa madogo madogo ambayo si yenye umaarufu mkubwa kiuchumi. Maziwa haya yanaweza kuonekana katika maeneo ya Ole na Kengeja.

Kutokana na kuwa na umbo la songombingo, kisiwa cha Pemba kina rasi na ghuba nyingi. Rasi maarufu ni zile za kigomasha, tvfkumbuu, Tundana, Gongoni, Makojuu na kadhalika. Mfano wa Ghuba ni Ghuba ya Wete, Chake Chake, Kiwani, Kwale na kadhalika

**HALI YA HEWA**

Pemba ipo katika ukanda wa joto. Kwa ujumla joto hutawala karibu miezi yote. Hata hivyo wataalamuwa hali ya hewa wameigawa miongo kama ifuatavyo :-

1. Kaskazi
2. Masika
3. Kipupwe
4. Vuli.

Kwa kiasi kikubwa miongo hii ndiyo inayoogoza shughuli za kilimo katika kisiwa hiki.

**KASKAZI**

Huu ni wakati ambao pepo huvuma kutoka kaskazini na kuelekea kusini kuanzia mwezi wa Disemba- Februari. Kwa kiasi kikubwa pepo hizi husababisha ardhi kukauka na pia jua huwa kali sana. Huu ni wakati wa joto kali katika mwambao mzima wa Afrika Mashariki. Watu wa kisiwa cha Pemba huitumia hali hii kutayarisha mashamba. Hii ni kwa sababu huu si wakati muafaka wa kilimo.

**MASIKA**

Upepo wa kaskazi husababisha mvua kubwa ambazo huanza mwezi wa Machi (21) hadi mei (21), mvua htzi hujulikana kama mvua za masika. Huu ni wakati ambapo wa kulima wa kisiwa cha pemba hulima mazao ya kudumu kama mikarafuu, minazi, miembe na kadhalika.

**KIPUPWE**

Huu ni mwongo unaoanza mwezi wa Juni (21) hadi Agosti (21). Hali ya hewa huwa ni ya baridi ya wastani kwa wageni, hata hivyo wenyeji wa kisiwa hiki huwa ni wakati wa baridi kali katika wakati huu, wakati huu huleta mvua ndogo ndogo zikiambatana na pepo baridi, mvua hizi hujulikana zaidi kama mvua za mchoo.

Hata hivyo mandhari ya kisiwa huwani yenye kuvutia sana wakatihuu, kwani miti huimarika kwa majani yaliyokoza kijani.

Wakulima hutumia wakati huu kwa kupanda mazao ya chakula kama viaza, mpunga, migomba, majimbi, na kadhalika.

**VULI**

Mwongo huu huanzia Septemba (21) hadi Novemba. Mvua ndogo ndogo hunyesha. Wakati mwengine mvua hizi huwa kubwa hadi kufikia milimita 80.

Hata hivyo huu huwa ni wakati muafaka kwa watu wa Pemba kulima mazao ya chakula kama migomba, mihogo na viazi.

**MIMEA YA ASILI**

Mimea ya asili ni miongoni mwa utajiri wa asili, mimea hii inaota wenyewe kulingana na uwezo wa ardhi (rutba) na hali ya hewa ya pahala husika.

Katika kila sehemu duniani ipo mimea inayokubaliana na mazingira ya mahali hapo. Pemba kwa upande wake tunaweza kugundua huwepo kwa misitu ya aina tatu kuu nazo ni :-

1. Misitu ya joto.
2. Misitu ya kisavana.
3. Misitu ya mikoko.

**MISITU YA JOTO**

Hii ni misitu inayoota kutokana na kuwepo kwa joto,pia hujulikana kama misitu ya kiikweta. Misitu hii huonekana kwa wingi katika sehemu ya mashariki ya kisiwa cha Pemba hasa sehemu 7..a Ngezi ambako aina mbali mbali za miti hupatikana na aina zenyewe ni kama mipera, mivule, mitondoo, michikichi na kadhalika.

Wenyeji huvuna miti hii kwa ajili ya kupata zana z.a ujenzi kama nguzo, boriti, mapau na mingine hufanywa mbao kwa ajili ya kutengeneza vyombo vya UVUVI.

**MISITU YA KJSAVANA**

Kwa kiasi kikubwa ukanda huu umetawaliwa na majani yenye urefu hadi kufikia mita moja. Majani maarufu katika ukanda huu ni vifaurogo (mimosa) na Pemba grass.

**MISITU YA MIKOKO**

Hii ni misitu inayoshamiri katika mwambao mzima wa kisiwa cha Pemba. Kuwepo kwa miti hii katika mwambao wa Pemba inatoa faraja kubwa kwa viumbe vya baharini.

Mikoko ni mazalia makubwa ya samaki kama pono, mikisi, chaa kadhalika pia kuna viumbe vyengine ambavyo vinaishi katika mazingira ya mikokoni. Mfano kaa uduvu na kadhalika.

Mikoko licha ya kuhuisha viumbe vya baharini pia imesaidia kupunguza monyoko wa ardhi pia huchangia ongezeka la mvua. Kutokana na kuwepo kwa mikoko Pemba inapata mvua nyingi hata kuliko visiwa vyengine vya mwambao wa Afrika mashariki.

**KILIMO**

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi changa. Kisiwa cha Pemba ambacho ni moja kati ya visiwa vikuu vinavyounda Jamhuri ya watu wa Tanzania Zanzibar. Karibu asili mia 90 imejikita na shughuli za kilimo kama njia kuu inayowawezesha watu wake kupata mahitaji yao ya lazima. Hii inatokana na kuvia kwa sekta ya viwanda ambayo inatoa ajira kubwa katika nchi za ulimwengu wa kwanza.

Kilimo katika kisiwa cha Pemba kinaweza kugawanya katika sehemu kuu. Nazo ni :-

1. Kilimo cha Chakula
2. Kilimo cha Biashara

Hiki ni kilimo ambacho hulimwa kwa lengo la kujitosheleza mahitaji ya chakula. Hii ni shuguli ya watu wengi wa Pemba. Kilimo hiki hulimwa wakati wa miongo ya k.ipupwe na vuli. Kutokana na rutba ya kisiwa cha Pemba mazao mengi husitawi. Mfano wa rnazao hayo ni ndizi, viazi vidogo vidogo, mpunga, muhogo. Pia wakulima hulima rniti ya matunda kama miembe, minazi mipapai, miti ya viungo kama milimao, midirnu na kadhalika.

Licha ya watu kujishughulisha na ukulima wa mazao ya chakula mahitaji ya chakula bado yamekuwa siyakujiosheleza. Hii ni

kwasababu chakula kikuu cha watu wa Pemba ni wali na ambao ukulima wake si wa kutosheleza kutokana na sababu mbili kuu :-

1. Eneo linalolirnwa mpunga ni <logo hii ni kutokana na ukweli kwamba mpunga hulimwa sehemu za mabondeni ambazo zinahifadhi maji kwa wingi. Licha ya hali hii sehemu kubwa ya kisiwa cha Pemba imeliwa na zao la karafuu hivyo sehemu ndogo tu ndiyoinayoweza hulirnwa karafuu.

2. Utaalamu duni wa ukulima. Ni wazi kuwa wakulima wa kisiwa cha Pemba wanatumia zana duni za kulima kama jembe la mkono, zanakama hii imepitwa na wakati na haiwezi kuleta Mapinduzi ya kilimo.

Pia wakulima hawana utaalamu wa kutosha bado wengi hawatumii mbolea. Pia kilimo cha umwagiiaji maji hakijapiga hatua nzuri yameendeleo. Hii labda inatokana na uwezo - mdogo wa Serikali kusimamia unazishwaji wa mashamba ya aina hii. Mara nyingi Serikali huar.zisha mashan1ba haya baada ya kupokea misaada kutoka kwa wahisani na mashirika ya kimataifa kama FAO na kadhalika. Siku zote misaada imekuwa si kitu cha kukitegemea katika maendeleo ya Nchi. Nyerere katika kitabu chake cha ujamaa anataha- dharisha kuhusu misaada kwa kuema kuwa rnisaada inahatarisha uhuru wa Nchi changa. Hapa anatoa hadhari kuwa watu wasitegemee misaada katika kupanga maeneo yao. Hivyo kutokana na sababu hizo Pemba iRa sehemu chache zinazolimwa kilirno cha umwagiliaji maji miongoni mwa sehemu hizo ni bonde la wema, mangwena katika mkoa wa kaskazini.

Pia kutokana uwezko mdogo wa Serikali matumizi ya zana za kisasa za kilimo kama matrekta ni mdogo. Mara nyingi Serikali hulazimika kupokea matrekta kwa njia ya msaada. Ni karibuni tumsaada kama huo ulitol.ewa kutoka Serikali ya china na korea.

Kwa upande mwengine watu wamekosa mwamko wa kutumia zana za kukokotwa na ngombe (plau) katika shughuli za kilimo. Pia hali hii imechangia na uwezo wa watu wenyewe kununua na kuzitumia zana hizo na pia serikali imeshindwa kuwashajiisha wakulima kuzitumia zana hizo kwa maendeleo ya kilimo.

Mbali na zao la mpurga wakulima mazao mengine ya chakula kama vile kunde, choroko, mahindi, mtama na mbaazi. Mazao haya hulimwa kwa wingi sehemu za vitongoji mkoa wa kusini, micheweni, maziwa ya ng'ombl.: ambao wao hulima zaidi mahindi na mtama.

**KILIMO CHA BIASHARA**

Kilimo cha biashara ni kile kilimo kinacholimwa kwa lengo la kuwapatia wata fedha iii kukidhia mahitaji yao. Pia kilimo hiki ndicho kinachoingizia tafia fedha za kigeni baada ya kuuzwa Nchi za nje. Katika shughuli hii Pemba inalima kwa wingi karafuu. Asilimia tisini (90) ya ardhi ya Pemba inalimwa karafuu.kwa sababu hiyo Pemba imekuwa ni roho ya uchumi wa Zanzibar kwani uchumi wa Zanzibar bado unategemea zao la karafuu.

Zao hii lilishamiri katika kisiwa cha Pemba tangu mwaka 1872 hii ni baada ya kutokea kimbunga kikubwa kilichofyeka kariba mikarafuu yote katika kisiwa cha Unguja. Abdul sharif anathibitisha haya katika kitabu Slaves Spices and Ivory in Zanzibar ukurasa wa 53-57. Mahitaji ya zao hili katika soko la dunia katika kame ya kumi na tisa iliimisha biashara ya urumiwa. Mikarafuu mingi ililimwa na watumwa na pia watumwa ndio walikuwa wavunaji wakubwa wa zao hilo. Mvunaji wa zao Ia karafuu huitwa kibarua.

Hata hivyo baada ya biashara ya utumwa kukomeshwa rasmi katikakame ya ishirini wazalendo wa visiwa hivi walishiriki kikamilifu katika uchumaji wa karafuu ushughulikia

Kwa ujumla.

Katika picha hii kijana wa kipemba anaonekana akichuma karafuu kwa kutumia kifaa maarufu pakacha.

Baada ya kuchumwa krafuu huanikwa kwenye jua kali kwa muda usiopungua siku tatu. Katika picha chini kijana anaonckana akianika karafuu. Karafuu huanikwa kwa kutumia kifaak ijulikanacho kama jamvi. Kwa kwaida karafuu huuzwa baada ya kukauka.

Kutokana na umuhimu wa zag hii kwa taifa, bado Serikali ynalimiliki zao hili kwa kutumia shirika lake Ia ZSTC Serikali la biashara Ia Zanzibar.

Karafuu huzaliwa mara mbili kwa mwaka. Mara hizo ni wakati wa mvua za vuli na mvua za masika. Wakati wa vuli karafuu nyingi huza!iwa kusini ya pemba. Kwa kwaida watl.l wa ( kusini) huvuna mwisho karafuu.

Karafuu nyingi huuzwa katika nchi za Indonesia.Singapore, na kadhalika. Baadae karafuu hupelekwa ulaya kutoka nchi hizi kama kiungo. Nchi zinazonunua karafuu duniani kwa matumizi ya viungo na madawa ni Ujerumani, marekani na kadhalika.

Hata hivyo zao hili limepoteza umaarufu wake duniani kiasi cha kuwa kosesha wazalishaji wa zao hili mori wa kuliendeleza zaidi. Hali hii imetokana na ushindaniwa mazao mengine ya viungo karna vile pilipili, tangawizi, na kadhalika. Kutokana na sababu hiyo bie ya zao hili imekuwa si ya kuaminika. Mara hupenda na mara hushuka hali inayosababisha hasara kubwa kwawazalishaji na wategemeaji wa zao hili.

**KAZI**

Kazi ni shughuli yoyote inayompatia mtu riziki yake. Aboud jumbe, Rais wa pili wa Zanzibar anasema "kazi ni uhai". Kari marx anasema "iii mwanadamu aweza kuishi lazima afanya kazi".

Tukichambua maelezo ya hapo juu tutaona kuwa midondoo yote yanakubali kuwa kazi ni kitu kisichoweza kuepukika katika maendeleo na uhai wa mwanadamu.

Kazi zinaweza kutafautika kutokana na mazingira na mwelekeo wa jamii husika. Kwa maana hiyo katika duni ya kisasa wanadamu hufanya kazi kwa lengo la kustawishi maisha yake na kuchangia katika maendeleo ya taifa lake.

Katika hali kama hiyo, watu wa pemba hujishughulisha na kazi mbali mbali kwa lengo la kukuza maisha yao na kuleta maendeleo ya taifa lao. Hivyo watu wa pemba hujishughulisha na kazi kuu zenyewe ni kama :-

1. Kilimo
2. Biashara
3. Kazi za ofisini.

**SHUGHULI ZA UVUVI**

Ni wazi kwa rnazingira ya kisiwa cha Pemba yanaifanya shughuli ya uvuvi kuwa ni miongoni mwa shughuli zinazowapatia watu riziki zao. Kutokana na uwezo wa kiuchumi kuwa mdogo watu wa Pemba hawajanufaika hasa na shughuli za uvuvi.

Hii ni kwasababu wavuvi hutumia zana duni za kuvulia kama vilemadema, nyavu ndogo ndogo, uzio na kadhalika.

Pia vyoma vinavyotumika havitoi fursa kwa wavuvi kuvua katika bahari kuu. Wavuvi wa pemba hutumia ngalawa. Mitumbwi, mashua, madau na kadhalika.

Mbali na haya utaalamu kwa wavuvini kikwazo kwa bado hawana ujuzi wala vifaa vya uhakika vya kuvulia. Hali hii inasababisha hazina kubwa ya samaki kubaki baharini na isitumike kama inavyotumiwa na jamii mfano: Peru, Japan, Urusi ambako wao uvuvi unachangia kipato cha nchi yao.

Hata hivyo, licha ya matatizo ya utaalamu karibu asilimia 20 ya watu wa Pemba wanaendesha maisha yao kwa kutegemea uvuvi. Jamii maarufu kwa shughli za uvuvi Pemba ni Wakojani.

**UFUGAJI**

Ufugaji ni shughuli nyengine inayofanywa na watu wa Pemba. Licha ya kuwa ufugaji ni shughuli kuu kwa baadhi ya nchi. Katika kisiwa cha Pemba watu hufuga na kukidhi mahitaji madogo madogo. Watu hawafugi kwa misingi ya kibiashara.

Hivyo watu wa Pemba hufuga wanyama kama Ng'ombe, Punda, Mbuzi, Kuku, Bata na kadhalika. Ng'ombe hufugwa kwa lengo la kupata nyama na kuwa saidia kubebea mizigo. Pia punda hufugwa kwa mantiki ya kuchukuwa mizigo.

Kwa kiasi kikubwa maumbeli ya kisiwa cha Pemba hulazimisha watu kutegemea ng'ombe au punda kwa shughuli za uchukuzi wa mizigu kutoka kijiji kimoja kwenda kingine.

Wanyama wengine kama bata, kuku mara nyingi hufugwa kwa chakula tu na sio biashara. Watu hufuga aina za ndege kwa misingi ya kufurahisha.

**BIASHARA**

Kisiwa cha Pemba watu hufanya biashara ndogo ndogo, wengine huuza na kununua bidhaa kutoka Unguja, Tanga, Mombasa na Dar es Salaam. Pia kuna maduka ya kutosha kwa biashara hasa katika sehemu za mijini kama vile Mkoani Chake Chake na Wete. Vile vile husafirisha baadhi ya mazao kama vile ndizi na kupeleka Unguja kwa vile ndiko mahali kwa biashara zaidi.

**HUDUMA ZA JAMII**

**BENKI**

Katika kisiwa cha Pemba watu huhitaji kuweka akiba zao katika Benki, hii ni kwa ajili ya usala.ma wa fedha zao kutokana na watu

wabaya kama vile wezi, kwa hali hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka matawi ya benki katika Wilaya ya Mkoani, Chake Chake, Wete na Micheweni iii wanachi wawe na uhakika wa usalama wa mali zao. Katika Benki hiyo watu huruhusiwa kuweka na kuchukua bila ya masharti ambayo yanaweza kusababisha kukosa pesa hizo.

**HOSPTALI**

Hospitali ni miongoni mwa huduma za jamii, hivyo imewajengea wananchi wake wa kisiwa cha Pemba hospitali takriban katika wilaya zote za Pemba na wananchi hupata huduma ya uzalishaji pamoja na uperesheni zote na ka.ma mgonjwa atakuwa na matatizo makubwa basi husafirishwa na kuletwa Unguja katika hospitali ya Mnazi mmoja ambayo ndiyo hospitali kuu. Vile vile bahati nzuri katika vijiji vingi vina kliniki za afya, mgawa tatizo ni la upungufu wa dawa katika kliniki hizo.

**ELIMU**

Kisiwa cha Pemba kimejaa skuli kuanzi skuli za msingi, sekondari mpaka vyuo. Kwa ufupi kila mwanafunzi, aliyefikia umri wa kwenda skuli sasa yuko skulini. Katika kisiwa cha Pemba kuna Chuo cha Ualimu, Chuo cha Kiislamu, Chuo cha Ufundi.

Hii yote ni juhudi ya Serikali baada ya kuona kuwa pana haja ya kuweza kufupisha au kupunguza ghara.ma zisizo za iazima kwa kuwasafirisha wanafunzi kuja Unguja kufuata elemu hata hivyo mwanafunzi anaweza kuhama na kuja Unguja kwa pale inapobidi.

**MAJI**

Maji ni huduma muhimu kwa maisha ya mwanadamu yoyote na yanapokosekana maji huwa ni matatizo makubwa sana. Kisiwa cha Pemba vile vile kina huduma za maji na bomba pamoja na visima, hivyo huduma hizi za maji zaidi hupatikana kwa nguvu za wananchi, Serikali kwa kupitia mpango wa TASAF.

Baadhi ya wakati kunakuwa na matatizo makubwa ya ukosefu wa maji hili ni tatizo ambalo linatokana na ukosekanaji wa umeme ambao husukuma mashine za maji, hata hivyo linapotokea tatizo kama hilo basi visima hutumika iii wanachi wapate maji.

**UMEME**

Umeme ni kiru muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku. Kisiwa cha Pemba hurumia umeme ambao unapatikana kwa kutumia jenereta, kwa sasa kisiwa cha Pemba kinakabiliwa na tatizo la wneme kwani mara kwa mara kunakuwa na tatizo la kukatika kwa umeme kwa sababu jenereta zilizopo ni za zamani, kwa hivyo mara kwa mara huhitaji matengenezo. Ingawa Serikali inajitahidi kufanya bidii iii kupunguza upungufu wa tatizo hilo kwa kufanya matengenezo ya mara kwa mara katika majenereta hayo.

**MAWASILIANO**

**BANDARI**

Kisiwa cha Pemba kina nadhari mbili ambazo ndizo zinazonnnika zaida, Bandari hizo ni Mkoani na \Vete. Bandari ya Mkoani ndio bandari kuu kuliko ya Wete kwani meli zote kwa sasa ndizo zinazoweza kutia nanga Mkoani lakini si meli zote ambazo zinaweza kutia nanga bandari ya wete, kwa hivi sasa meli ya Aziza na kasa ndizo an1bazo zinazoweza kutia nanga. Watu hutumia usafiri wa meli, ngalawa, jahazi na boti kusafiri kwenda sehemu mbali mbali kutoka Pemba, kwa mfano kwenda Tanga, Unguja, Mombasa,Dar es Salaam na kadhalika.

**KIWANJA CHA NDEGE**

Kisiwa cha Pemba kuna kiwanja cha ndege kimoja ambacho kiko Chake Cake. Hiki si kiwanja kikubwa sana hivyo ndege ambazo zinatua na kuruka ni ndege ndogo ndogo. Kwa maana hiyo ndege za kukodi kama vile chata au Fokker ndizo ambazo huruka na kutua katika kiwanja hicho.

**USAFIRI WA NDANI**

Walsh, M. T., (2009), The Use of Wild and Cultivated Plants as Famine Foods on Pemba Island, Zanzibar (unpublished

Kuna usafiri wa ndani ambao kisiwa cha Pemba wanachi huwa wanautumia hivyo vyombo kama gari, pikipiki (Honda) skuta, baiskeli, ng'ombe na punda.

Kwa vile wanaomiliki gari au vyombo vya moto ni kidogo kutokana na uwezo wa wananchi sasa kuna mpango maalum ambao watu wanatumia, nao huitwa dala dala, hivyo watu hutozwa pesa iii kupanda gari hizo na mtu kwenda anakotaka kwa urahisi.

Vile vile vyombo kama pikipiki na baiskeli ni matumizi ya mtu mmoja. Hata hivyo watu wengine hutumia ng'ombe na punda kwa kuchukulia mizigo yao na kwa ajili ya usafiri.

**BARABARA**

Kisiwa cha Pemba kina barabara, lakini barabara na mjini ndio nzima na baadhi ya barabara za vijijini. Hivyo barabara kutoka Mkoani hadi Chake Chake na Chake Cake hadi Wete ndiyo nzima na bara ya wingwi pia kuna barabara zonazoendelea na kujengwa ikiwemo ile ya mtu haliwa Mkoani.

**MWASILIANO YA SIMU**

Kisiwa cha pemba kina mwasiliano ya kutosha ya simu za mkoani kama vile Zantel na TICL. Kwa hivyo wanachi hawana shida ya kupata mwasiliano wakati wowote.

**UTALII**

Kisiwa cha Pemba vile vile hakiko nyuma katika shughuli za utalii, kuna hoteli za kitalii kama vile Mkoani na Chake Chake na Wete, watalii wanapofika Pemba hupenda kutembelea sehemu za historia ili kuona ndege na wanyarna mbali mbali wa kuvutia, pia hupenda kuona magofu ua Mkama Ndume, Kisiwa cha Mesali, Mkumbuu, Msitu wea Ngezi pamoja na bahari. Sasa Serikali inajaribu kuimarisha sehemu mbali mbali kwa ajili ya utalii. Vile vile watalii hupenda kutaka kuona na kuonja viungo vya aina mbali mbali pamoja na kuzarnia baharini iii kuangalia viumbe hai.

**MAREJEO**


Abdallah, H. B., (2013), Dola Kongwe ya Zanzibar Kutoka Omani hadi Kongo, Dar es Salaam: Kauthar Printers

Al-Zumor, A. Q. G., (2009), A Social-Cultural and Linguistic Analysis of Yemeni Arabic Personal Names, Abha: King Khaled University.

BAKIZA (2008), Utamaduni wa Mzanzibar, Zanzibar: Quark Xpress Printing Services.

BAKIZA (2010), Kamusi la Kiswahili Fasaha, Nairobi: Oxford University Press.

El-Hawi, F. F., (2014), ―Mchango wa Majina ya Mitaa na Koo za Mji wa Bagamoyo katika Kuchunguza Asili na Historia ya Waswahili‖, Ripoti ya Utafiti kwa Ajili ya Kukamilisha Masomo ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro (Haijachapishwa).

Faki, H. H., (2010), ―Utambulisho wa Koo za Watu wa Pemba Kupitia Majina ya Watu: Micheweni Pemba‖, Ripoti ya Utafiti kwa Ajili ya Kukamilisha Masomo ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro (Haijachapishwa).

Kipacha, A. na Kombo, I., (2009), Dunia Kokwa ya Furu: Amali ya Misemo ya Kipemba, katika Jounal of Humanities, Juzuu 1 (1), Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma

Mlacha, S., (2008), "Fasihi Simulizi na Usuli wa Historia ya Pemba‖ katika Mlacha, S. na Hurskainen, A. (Wah.) Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili, Dar es Salaam: TUKI na Chuo Kikuu cha Helsinki..

Sengo, T. S. Y., (2012), Sengo na Fasihi za Kinchi. Al-amin Education and Research
Academy: Dar es Salaam.